MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

# JARIDA LA HALI YA HEWA

*Na. 38 Toleo maalumu: Utabiri wa mvua za Machi hadi Mei (MAM) 2025* *Umetolewa Tarehe 23 Januari 2025*

## MUHTASARI

- Mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo ya pwani ya kaskazini (kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mkoa wa Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Dar es Salaam, Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), kaskazini mwa mkoa wa Kigoma na ukanda wa Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga na magharibi mwa mikoa ya Simiyu na Mara). Aidha, Mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya nyanda za juu kaskazini mashariki pamoja na mashariki mwa mikoa ya Mara na Simiyu.
- Mvua za Masika zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Machi, 2025 katika maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria na pwani ya kaskazini; na katika wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Machi, 2025 katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki.
- Ongezeko la mvua linatarajiwa mwezi Aprili, 2025.
- Vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi pamoja na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri ukuaji wa mazao hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani.
- Kina cha maji katika mito na mabwawa kinatarajiwa kuongezeka hivyo kuongeza hatari ya mafuriko hususan katika maeneo yanayoathiriwa na mafuriko.
- Magonjwa ya mlipuko yanaweza kujitokeza kutokana na uchafuzi wa maji.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MACHI HADI MEI, 2025

Kwa kipindi cha mvua za msim wa Masika 2025, joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi ikilinganishwa na upande wa magharibi mwa Bahari ya Hindi (Pwani ya Afrika Mashariki). Hali hii inatarajiwa kupunguza kasi ya msukumo wa unyevunyevu kutoka Bahari ya Hindi kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi. Eneo la Tropiki ya Kati ya Bahari ya Pasifiki, linatarajiwa joto la Bahari la chini kidogo ya wastani. Vilevile, joto la bahari la wastani linatarajiwa katika eneo la pwani ya kusini mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (Pwani ya Angola). Hali hii kwa pamoja inatarajiwa kudhoofisha mifumo inayosababisha mvua katika msimu huu.

Kwa upande mwingine, upepo katika Ziwa Victoria unatarajiwa kuvuma kutoka magharibi. Hali hii inatarajiwa kuimarisha kidogo mifumo nayosababisha mvua katika maeneo yaliyopo upande wa mashariki mwa Ziwa Victoria na nyanda za juu kaskazini mashariki.

## MWELEKEO WA MVUA ZA MASIKA, 2025

Msimu wa mvua za Masika ni mahususi kwa maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), pwani ya kaskazini (kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mkoa wa Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Dar es Salaam, Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), ukanda wa Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu na Mara) pamoja na kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma. Kutokana na mifumo ya hali ya hewa inayotarajiwa katika kipindi cha Masika mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya nyanda za juu kaskazini mashariki pamoja na mashariki mwa Mikoa ya Mara na Simiyu. Aidha, mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo ya pwani ya kaskazini, kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma na ukanda wa Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga na magharibi mwa mikoa ya Simiyu na Mara) katika kipindi cha Msimu wa Masika, 2025. Ongezeko la mvua linatarajiwa mwezi Aprili, 2025. Maelezo ya kina juu ya mwelekeo wa mvua za msimu ni kama ifuatavyo:

***Kanda ya Ziwa Victoria: (mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, na Mara) pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma (wilaya za Kakonko na Kibondo)***


Mvua za Masika zinatarajiwa kuwa za Wastani hadi Chini ya Wastani katika maeneo mengi ya ukanda wa Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga na magharibi mwa Mikoa ya Simiyu na Mara) pamoja na kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma. Katika maeneo ya mashariki mwa Mikoa ya Mara na Simiyu mvua zinatarajiwa kuwa za Wastani hadi Juu ya Wastani. Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Machi na kuisha wiki ya kwanza ya mwezi Mei, 2025.

***Ukanda wa Pwani ya kaskazini: (kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mkoa wa Pwani (ikijumuisha kisiwa cha Mafia), Dar es Salaam, Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba)***

Mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya ukanda wa pwani ya kaskazini. Mvua hizo zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Machi na kuisha wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Mei, 2025

***Nyanda za juu kaskazini mashariki: (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro)***

Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuwa za Wastani hadi Juu ya Wastani na zinatarajiwa kuanza wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Machi na kuisha wiki ya kwanza ya mwezi Mei, 2025.




Kielelezo: Mwelekeo wa mvua za Masika, 2025

***Angalizo 1**: Izingatiwe kuwa matukio ya hali mbaya ya hewa ikiwemo vipindi vya mvua kubwa yanaweza kujitokeza hata katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani.*

## ATHARI NA USHAURI

**Sekta za Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Maji**

Kwa upande wa kilimo, vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi pamoja na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri ukuaji wa mazao katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani. Vilevile, wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea yanayoendana na hali ya ongezeko la unyevu kama vile ukungu yanatarajiwa kuongezeka na kuathiri mazao kama ndizi, mahindi, mpunga, mihogo na maharage. Hata hivyo hali ya upungufu wa unyevu inaweza kujitokeza hasa katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani. Hali hii inaweza kupelekea athari katika ukuaji wa mazao ya kilimo.

Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa kuzingatia hali ya unyevu katika udongo, kutumia mbinu bora na teknolojia za kuzuia maji kutuama shambani, kuhifadhi maji shambani, kuzuia mmomonyoko na upotevu wa rutuba kutokana na kutuwamisha maji kwa muda mrefu au mafuriko.

Aidha, inashauriwa kuimarisha miundombinu ya kilimo na kudhibiti kwa wakati magonjwa ya mimea na wadudu waharibifu ili kupunguza madhara yanayoweza kujitokeza. Wakulima wanashauriwa kutafuta taarifa sahihi kutoka kwa maafisa ugani kwa kuzingatia utabiri wa msimu wa wilaya husika katika kuchagua mbegu na zao sahihi.

Aidha, wakulima na maafisa ugani wanashauriwa kuendelea kutumia utabiri wa siku na siku kumi ili kufuatilia kwa ukaribu mwenendo wa utabiri wa msimu.

Kwa upande wa mifugo, maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani, wafugaji na wavuvi wanatarajiwa kunufaika na upatikanaji wa malisho, maji na chakula cha samaki.

Hata hivyo, milipuko ya magonjwa ya mifugo kama vile homa ya bonde la ufa, ugonjwa wa miguu na midomo, na kuzaliana kwa wadudu wadhurifu kunaweza kujitokeza.

Upungufu wa maji unaweza kujitokeza katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani na hivyo unaweza kuathiri upatikanaji wa maji na malisho ya mifugo na kusababisha migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Wafugaji wanashauriwa kuweka mipango mizuri ya matumizi na uhifadhi wa maji na vyakula vya mifugo. Aidha, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kutumia taarifa za utabiri wa hali ya hewa na kuzingatia ushauri unaotolewa na maofisa ugani ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza na kuendelea kunufaika na hali ya hewa inayotarajiwa wakati wa msimu.

Kupungua kwa kina cha maji katika mito, mabwawa na hifadhi ya maji ardhini kunatarajiwa kujitokeza hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani. Ongezeko la vina vya maji katika mabwawa na mito linatarajiwa kujitokeza hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani na hivyo kupelekea kuongezeka kwa matukio ya mafuriko hususan katika maeneo anayoathiriwa zaidi na mafuriko.

Upungufu wa maji unaweza kupelekea ongezeko la gharama za kutibu maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani. Matumizi endelevu ya rasilimali maji yanasisitizwa hususan katika shughuli za umwagiliaji.

***Angalizo 2:** Mwelekeo wa mvua uliotolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha mvua za Masika (miezi mitatu) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya mvua na mabadiliko ya muda mfupi vitazingatiwa katika utabiri wa kila siku na utabiri wa kila mwezi. Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia taarifa za utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi na tahadhari kama zinavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)*